

NAMNA MBINU YA KIKUNDI CHA KUJIFUNZA CHA FAMILIA ZA WAKULIMA (FFLG) INAVYOFANYA KAZI



Mbinu shirikishi ya kujifunza, kufanya na kubadilishana uzoefu kwa ajili ya kuboresha uzalishaji na maisha ya familia za wakulima.

Imeandaliwa na Shirika la Kilimohai Tanzania (TOAM)

Utangulizi kuhusu kipeperushi hiki

Kipeperushi hiki ni toleo rahisi na lenye lugha nyepesi la Mwongozo wa Mbinu ya Kikundi cha Kujifunza cha Familia za Wakulima (Farmer Family Learning Group - FFLG). Kimeandaliwa kwa ajili ya wadau mbalimbali wa kilimo, wakiwemo wakulima, wawezeshaji, taasisi za wakulima, mashirika ya maendeleo, wataalamu na wadau wengine wanaotaka kuelewa kwa urahisi dhana na namna ya kutumia mbinu ya FFLG.

Toleo hili linatoa muhtasari wa dhana, misingi na namna ya kutumia mbinu ya FFLG kwa lugha rahisi na yenye msisitizo wa vitendo, ili iwe rahisi kusoma, kuelewa na kutumia katika shughuli za kujifunza na kusambaza maarifa kwa wakulima.

Kipeperushi hiki kimeandaliwa kupitia Mradi wa Kitovu cha Maarifa ya kilimo ikolojia hai Afrika Mashariki (Knowledge Hub for Organic Agriculture and Agroecology East Africa - KHEA), kwa lengo la kuwezesha upatikanaji na matumizi ya maarifa ya kilimo ikolojia hai kwa wadau mbalimbali.

Toleo hili la Kiswahili linapatikana katika jukwaa la kidijitali la KCOA: KCOA Africa - Knowledge Platform

Kwa msomaji anayehitaji maelezo ya kina, Mwongozo kamili wa FFLG unaweza kutafutwa kwenye jukwaa hilo kwa kutumia neno "FFLG Guide."

Shukrani na utambuzi

Mwongozo kamili wa FFLG unaofahamika kama "FFLG Guide" uliandaliwa chini ya Programu ya ESFROMA, kupitia uratibu wa KOFLEC. Mwongozo huo ndio uliotumika kama chanzo kikuu cha toleo hili.

Kupitia Mradi wa KHEA, kazi ya kutafsiri, kurahisisha maudhui na kuzalisha toleo hili maarufu la Kiswahili imewezeshwa ili kuwafikia wasomaji wengi zaidi katika Afrika Mashariki, hususan wadau wanaotumia Kiswahili katika kujifunza na kusambaza maarifa.

Nini maana ya mbinu ya FFLG?

Kikundi cha Kujifunza cha Familia za Wakulima (FFLG) ni mbinu shirikishi ya kujifunza kwa kufanya, ambapo familia za wakulima hukutana, hutembeleana katika mashamba yao na kujifunza kutokana na uzoefu wao wenyewe na wa wakulima wenzao. Kwa mwongozo wa mwezesaji, familia hujadili changamoto zinazowakabili na kwa pamoja hutafuta na kujaribu suluhisho zinazofaa kwa mazingira na rasilimali zilizopo katika mashamba yao.

FFLG inaangalia familia ya mkulima kama kitengo cha kilimo, hivyo wanafamilia mbalimbali hushiriki katika shughuli za shamba, kujifunza na kufanya maamuzi kulingana na uwezo na nafasi zao. Kujifunza hakufanyiki darasani pekee; shamba lenyewe linakuwa sehemu muhimu ya kujifunzia, kupitia ziara, majaribio, majadiliano na kubadilishana uzoefu.

Kikundi cha FFLG Inatofautianaje na kikundi cha kawaida?

FFLG ni zaidi ya kuwa na kikundi cha wakulima wanaokutana pamoja. Ni mfumo wa kujifunza kwa vitendo, ambapo familia za wakulima hutumia uzoefu, mashamba yao na rasilimali zilizopo kama sehemu ya kujifunzia na kutafuta suluhisho.

Kikundi cha kawaida	FFLG
Kinaweza kukutana kwa ajili ya mikutano au shughuli maalum	Kujifunza na kufanya kwa vitendo ni msingi wa FFLG
Wakulima wanaweza kujifunza kutoka kwa mtaalamu au mwezesaji	Wakulima wanajifunza pia kutokana na uzoefu wa wenzao na mashamba yao
Shughuli zinaweza kufanyika katika eneo moja la pamoja	Wanachama hutembeleana katika mashamba ya familia mbalimbali
Mkazo unaweza kuwa kwenye shughuli au kazi ya pamoja	Mkazo ni kujifunza, kupanga, kufanya, kutathmini na kuboresha
Familia inaweza kutoshirikishwa kama kitengo kimoja	Familia nzima na wanafamilia hushiriki kulingana na uwezo na nafasi zao
Suluhisho linaweza kutafutwa kutoka nje	FFLG inasisitiza kwanza kutambua na kutumia rasilimali na fursa zilizopo ndani ya mashamba na katika mazingira ya

Kwa nini wakulima watumie mbinu ya FFLG?

FFLG inalenga kuwasaidia wakulima kujifunza kutokana na uzoefu wao wenyewe na wa wakulima wengine, kufanya maamuzi kwa pamoja na kuboresha shughuli za kilimo kulingana na mazingira na rasilimali walizonazo. FFLG inaweza kusaidia katika maeneo yafuatayo:

1. Kuboresha uzalishaji wa shamba

Familia hujifunza kuhusu usimamizi wa udongo, mazao, mifugo, mbegu na mipango ya shamba, kwa kuangalia changamoto halisi zilizopo katika mashamba yao.

2. Kujifunza kutoka kwa wakulima wenzao

Kupitia ziara za mashambani, mkulima anaweza kuona kwa vitendo kile ambacho mkulima mwingine anafanya, kujadili matokeo na kubadilishana uzoefu.

3. Kuimarisha ushiriki wa familia

FFLG huichukulia familia kama kitengo cha kilimo. Wanafamilia hushiriki katika shughuli za shamba, kujifunza na kuchukua majukumu kulingana na uwezo wao.

4. Kujenga shamba lenye uwezo wa kukabiliana na changamoto

FFLG inahimiza mambo kama mseto wa mazao na mifugo, uhifadhi wa udongo na maji, mipango jumuishi ya shamba na mabadiliko kuelekea kilimo hai.

5. Kuongeza fursa za kiuchumi

Familia na vikundi vinaweza kujifunza kuhusu uongezaji thamani, masoko ya pamoja, kuweka akiba na kupata huduma kulingana na mahitaji yao.

6. Kuboresha lishe ya familia


Uzalishaji wa mazao mbalimbali unaweza kusaidia familia kupata chakula cha aina mbalimbali na lishe bora.

7. Kuimarisha mshikamano katika jamii

FFLG inaweza pia kuchochea hatua za pamoja zinazowanufaisha wakulima na jamii kwa ujumla, kama kushughulikia changamoto za mazingira au kusaidiana katika mahitaji ya jamii.

FFLG Inafanyaje Kazi?

FFLG hufanya kazi kupitia kujifunza kwa vitendo, ambapo familia za wakulima hujifunza pamoja na kutumia mashamba yao na uzoefu wao kama sehemu ya kujifunzia.



Kumbuka: Katika FFLG, kujifunza hakutenganishwi na shughuli halisi za mkulima. Shamba la familia linakuwa sehemu muhimu ya kujifunzia, na uzoefu wa

Ziara na Mzunguko: Shamba linakuwa shamba darasa

Moja ya vipengele muhimu vya FFLG ni familia za wakulima kutembeleana katika mashamba yao. Ziara hizi hutoa nafasi ya kujifunza moja kwa moja kutokana na kile kinachofanyika katika shamba la familia mwenyeji

Ziara za mzunguko ni nini?

- Ni utaratibu ambapo familia za FFLG hutembeleana kwa zamu katika mashamba yao. Kikundi hupanga mapema shamba litakalotembelewa na mambo yatakayojadiliwa au kujifunzwa.
- Ziara hizi zinaweza kufanyika takribani mara nne kwa mwezi, kwa kutembelea mashamba mbalimbali ya familia wanachama

Shughuli zinazoweza kufanyika wakati wa ziara

- Kuangalia shughuli zinazofanyika katika shamba la familia.
- Kujadili changamoto zinazojitokeza katika shamba hilo.
- Kuuliza maswali na kubadilishana uzoefu.
- Kuangalia njia ambazo familia imetumia kukabiliana na changamoto.
- Kujifunza kutokana na kile kinachoonekana kwa vitendo.
- Kukubaliana hatua au mambo ya kuendelea kuyafuatilia.

Familia mwenyeji nayo inajifunza

- Ziara si kwa ajili ya kuwakagua wakulima.
- Familia mwenyeji inakuwa sehemu ya mchakato wa kujifunza.
- Wanafamilia hushiriki katika kupokea kikundi, kueleza uzoefu wao na kujadili kile kinachofanyika katika shamba lao.

Kumbuka: Ziara za mzunguko zinapaswa kuongozwa na mpango wa kikundi, ili kila ziara iwe na lengo la kujifunza na kuchangia katika maendeleo ya familia na kikundi.

Nani anashiriki katika FFLG?

FFLG inalenga familia za wakulima wadogo, hasa wale wenye rasilimali chache na wanaokabiliwa na changamoto mbalimbali za uzalishaji na mazingira. Katika FFLG, familia haichukuliwi kama mtu mmoja, bali kama kitengo cha kilimo kinachojifunza na kufanya kazi pamoja

1. Familia za wakulima

- Familia ndiyo msingi wa FFLG. Wanafamilia hushiriki katika shughuli za shamba, kujifunza na kuchukua majukumu kulingana na uwezo na nafasi zao.

2. Wakulima wenzao

- Kila familia ni mwanafunzi na pia chanzo cha maarifa.
- Kupitia ziara na majadiliano, wakulima hushirikishana uzoefu, changamoto na njia walizotumia katika mashamba yao.

3. Mwezeshaji

- Mwezeshaji husaidia kuwezesha mchakato wa kujifunza.
- Jukumu lake si kuwaambia wakulima kila kitu cha kufanya, bali kuleta pamoja mitazamo, maarifa na uzoefu mbalimbali ili wakulima wajadili na kukubaliana hatua wanazomiliki na wanaoweza kuzibadilisha kulingana na hali yao halisi.

4. Jamii inayozunguka

- FFLG inaweza pia kuchangia maendeleo ya jamii pana kupitia hatua za pamoja.
- Mifano ya shughuli kama kusaidia kuboresha njia za kusafirisha mazao, kusaidia wazee kuzalisha mazao yenye lishe, kusaidia elimu ya vijana na kuboresha ufugaji.

Kanuni muhimu


- Kila mwanafamilia ana nafasi ya kujifunza na kuchangia.
- FFLG inazingatia pia majukumu ya kijinsia na ushiriki wa wanafamilia mbalimbali, kwa lengo la kuhakikisha kuwa familia inamiliki mchakato na kwamba maendeleo ya shamba yanaweza kuendelea kutoka kizazi kimoja hadi kine

Nafasi ya mwezeshaji

Katika FFLG, mwezeshaji ana nafasi ya kuwezesha mchakato wa kujifunza, si kuwa chanzo pekee cha majibu. Mwezeshaji husaidia kuleta pamoja mitazamo, maarifa na uzoefu wa wakulima ili wajadili changamoto zao na kukubaliana juu ya hatua zinazofaa kwa mazingira yao.

Mwezeshaji anasaidia:

- Kufungua majadiliano na kuhakikisha washiriki wanapata nafasi ya kutoa mawazo yao.
- Kusikiliza uzoefu wa wakulima na kutumia uzoefu huo kama sehemu ya kujifunza.
- Kuuliza maswali yanayochochea fikra badala ya kutoa majibu yote.
- Kusaidia kikundi kuchambua changamoto na kutafuta suluhisho linalowezekana.
- Kuwezesha kujifunza kwa vitendo kupitia ziara, maonyesho na shughuli za shambani.
- Kuunganisha maarifa na uzoefu mbalimbali ili kikundi kiweze kufanya maamuzi kwa pamoja.
- Kusaidia kikundi kutathmini na kuboresha yale wanayofanya.



Mwezeshaji si "mwalimu wa kila kitu". Mwezeshaji anaongoza mchakato; wakulima wanamiliki maarifa, maamuzi na hatua wanazokubaliana kuchukua.

Jinsi ya Kuanzisha na kuendesha FFLG

FFLG inahitaji maandalizi mazuri, ushiriki wa familia na mchakato unaoendelea wa kujifunza. Mwongozo unaeleza umuhimu wa kuunda, kutekeleza na kuimarisha FFLG, huku mwezeshaji akiwa na nafasi muhimu katika kuanzisha na kusaidia mchakato huo.



FFLG haimaliziki baada ya mafunzo. Kujifunza kunaendelea kadiri familia zinavyofanya, kujaribu, kutathmini na kubadilishana uzoefu.

Kumbuka: Hizi ni hatua zilizorahisishwa kwa ajili ya matumizi ya maarifa ya KHEA; hazipaswi kuchukuliwa kama orodha rasmi ya hatua kwa hatua iliyonukuliwa moja kwa moja kutoka kwenye mwongozo.

Mfano wa ziara ya shambani:

Ziara ya shambani ni nafasi ya kujifunza moja kwa moja kutoka kwenye shamba la familia. FFLG inasisitiza ziara zilizopangwa mapema na zinazolenga kujifunza kutokana na uzoefu wa familia mwenyeji. Huu ni mfano wa namna ziara inaweza kuendeshwa; ratiba inaweza kubadilishwa kulingana na mahitaji ya kikundi.

1. Kuwasili na kujitambulisha

Familia mwenyeji inawakaribisha washiriki na kueleza kwa kifupi shughuli zinazofanyika kwenye shamba.

2. Kutazama shamba

Washiriki wanazunguka shambani na kuchunguza shughuli, mazao, mifugo au changamoto zinazohusiana na mada ya ziara.

3. Familia kueleza uzoefu wake

Familia mwenyeji inaeleza kile inachofanya, changamoto ilizokutana nazo na uzoefu iliyopata.

4. Maswali na majadiliano

Wakulima wanauliza maswali, kutoa uzoefu wao na kujadili kile walichokiona.

5. Kujifunza kwa vitendo

Kikundi kinaweza kufanya au kuoneshwa kwa vitendo shughuli inayohusiana na mada ya ziara.



6. Kutafakari na kukubaliana hatua

Kikundi kinajadili: Tumejifunza nini? Tunaweza kutumia nini katika mashamba yetu? Ni jambo gani tunahitaji kufuatilia zaidi?

Mfano wa maswali ya kutumia wakati wa ziara

- Tunaona nini katika shamba hili?
- Familia imefanya nini ili kukabiliana na changamoto hii?
- Ni nini kimefanya kazi vizuri?
- Ni changamoto gani bado ipo?
- Tunaweza kujifunza nini kutokana na uzoefu huu?
- Ni hatua gani tunaweza kujaribu katika mashamba yetu?

Jinsi FFLG inavyoweza kuleta mabadiliko katika familia na jamii

FFLG haishughulikii uzalishaji wa shamba pekee. Mbinu hii inaangalia familia, kikundi na mazingira yanayowazunguka kama sehemu zinazohusiana. Kwa hiyo, kujifunza na kufanya kazi pamoja kunaweza kuleta mabadiliko katika ngazi mbalimbali.

1. Ngazi ya familia

- FFLG huimarisha familia kama kitengo cha kilimo. Wanafamilia hushiriki katika shughuli za shamba na kujifunza kuchukua majukumu kulingana na uwezo wao.

Hii inaweza kusaidia familia:

- kupanga shughuli za shamba kwa pamoja;
- kuongeza utofauti wa mazao na shughuli za kilimo;
- kuboresha usimamizi wa udongo na maji;
- kuimarisha uzalishaji wa chakula na lishe;
- kujenga umiliki wa pamoja wa maendeleo ya shamba.

2. Ngazi ya kikundi

Familia zinapojifunza pamoja, zinaweza pia kufanya shughuli za pamoja kama:

- kuongeza thamani ya mazao;
- kutafuta masoko;
- kujenga uwezo wa taasisi za wakulima;
- kushirikiana katika kutatua changamoto zinazowahusu.

3. Ngazi ya jamii na mazingira

- Kwa kuwa familia za FFLG kwa kawaida zinapatikana katika eneo moja, zinaweza kuchukua hatua zinazohusisha mazingira yao kwa pamoja.
- Mfano wa hatua za pamoja zinazoweza kusaidia kupunguza mmomonyoko wa udongo, kupunguza uchafuzi wa maji na kuboresha mazingira.
- FFLG inaweza kujenga mtaji wa kijamii kupitia kusaidiana katika shughuli zinazowanufaisha watu wengine katika jamii.

Hitimisho

FFLG ni mbinu inayowaleta familia za wakulima pamoja ili kujifunza, kufanya na kuboresha. Badala ya kutegemea maarifa kutoka nje pekee, FFLG hutumia uzoefu wa wakulima, mashamba yao na rasilimali zinazopatikana katika mazingira yao kama sehemu ya kujifunza.

Kupitia ziara za mashambani, majadiliano, vitendo na kubadilishana uzoefu, familia huweza kutambua changamoto zao, kutafuta suluhisho linalofaa na kuendelea kuboresha shughuli zao za kilimo.

FFLG pia huimarisha ushiriki wa familia, ushirikiano wa wakulima na hatua za pamoja zinazoweza kuchangia maendeleo ya jamii na utunzaji wa mazingira.